# SURA

# YA KWANZA

## I. Historia fupi ya Maisha ya Muhammad (S.a.w)

A. Nasaba yake. Ina aminika kuwa Muhammad alitokea katika nasaba ya Ibrahimu ambaye aliyekuwa anaishi Kanaani Palestina maelfu ya miaka kabla ya Muhammad, inaaminika katika kizazi cha mmoja wa watoto wake aliyemzaa kupitia mjakazi (mtumwa) aitwaye Hajiri ambaye alikuwa Mmisri.

Kwa mujibu wa nukuu kutoka **kwa Shekhe Othman Maalim wa Islamic Faundation Zanzibar** Katika kitabu chake kiitwacho Historia ya Mtume. Ukurasa wa 5 Sura ya Kwanza, kipengele cha 1. Kisemacho Nasaba ya Mtume. Amelezea kwamba, nasaba ya Bwana Mtume Muhammad (s.a.w) inatokana na kizazi cha nabii Ibrahimu (a.s) …….aliyemuoa mwanamke wa Kimisri aitwaye Haajra….akazaa mtoto akamwita Ismail.

Kwa mujibu wa maelezo ya Shekhe Othman, alielezea mfululizo wa vizazi hivyo, ambavyo inasemekana Ismail aliwazaa hao kutoka mke wa pili aliyeshauriwa na Ibrahimu kwamba aoe mke mwingine. Nasaba hiyo ni vizazi 12 navyo ni hivi, kutoka Ismail hadi nabii Muhammad kama ifuatavyo.

**Orodha:**

1. Banalut
2. Adhail
3. Mubsham
4. Mishmaa
5. Dumana
6. Misha
7. Hada
8. Yitma
9. Ytur
10. Nafiys
11. Qaidam
12. Qaidar

Inaaminika katika orodha hiyo mtoto wa Ismail aliyetokea nabii Muhammad katika vizazi vyake alikuwa ni wa 12 aitwaye QAIDAR

**Ukoo wa Muhammad.**

***Muhammad bin Abdillah bin Abdul Mutwalib bin Hashim bin Abdi Manaf bin Qusway bin Kiilaab bin Murrah bin Kaab Bin Luayy Bin Ghalib Bin Fihr Bin Malik Bin Nadhir Bin Kinanah Bin Khuzaymah Bin Mudrikat Bin Ilyas Bin Mudhwar Bin Nizar Bin Maad Bin Adnaan, ambaye ni kizazi cha Qaidar ambaye naye ni mtoto wa Ismail ambaye pia ni mtoto wa nabii Ibrahimu.***

*B.* **Nukuu ya vizazi vya Ishmael kwa mujibu wa Biblia na imani ya Kikristo na Wayahudi.**

1. **Kwa mujibu wa Biblia,** na kwa mujibu wa historia ya vitabu vya nyuma ya Quran na maelezo ya Mtume Muhammad.

Ibrahimu alikuwa na mke mmoja aitwaye Sara Mwanzo 17:15.*16 Mungu akamwambia Ibrahimu,* ***Sarai mkeo,*** *hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake* ***litakuwa Sara.*** *Nami nitambariki, na tena*

*nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake.*

Kwamba alikuwa na mjakazi (Mtumwa) aitwaye Hajiri Mwazo 16:1. *Basi Sarai mkewe Abramu hakumzalia mwana, naye alikuwa na mjakazi, Mmisri, jina lake Hajiri*.

Katika Mwanzo 16. Sara aliongea na Ibrahimu ili aingie kwa Hajiri ili wapate mtoto. Kwa desturi za wakati huo, mjakazi au mtumwa akizaa chini ya bibi yake, huyo mtoto atakuwa wa bibi (bosi) na bosi mwanamke ndiye mwenye mamlaka na maamuzi juu ya mjakazi wake na mtoto. Hii inarejea hata kwenye kisa cha Musa kuokotwa na binti Farao Musa aliitwa mwana wa binti Farao. Nukuu ya Biblia Mwanzo 16:1 *Sarai akamwambia Abramu, Basi sasa, Bwana amenifunga tumbo nisizae, umwingilie mjakazi wangu* ***labda nitapata uzao kwa yeye****. Abramu akaisikiliza sauti ya Sarai.*

Rejea maneno haya "***labda nitapata uzao kwa yeye****.*"

Kwa mujibu wa historia za mababa wa kale wa imani kwa desturi zao za kawaida, huwa mwanamke anapoolewa, huwa anapewa mtumwa au mjakazi wake atakayemtumikia maisha yake yote, Rejea Mwanzo 24:61 ***Rebeka akaondoka na vijakazi wake****, nao wakapanda juu ya ngamia, wakamfuata yule mtu. Naye huyo mtumishi akamchukua Rebeka akaenda zake.*

Rejea maneno haya "***Rebeka akaondoka na vijakazi wake"*** Hivyo basi, ni wazi kuwa, kwa desturi za mabibi wengi wa kiungwana haswa wale walio matajiri katika koo zao, wazazi wao huona fahari kuwaoza watoto wao na kisha kuwapatia watumishi (au watumwa) wa kuwatumikia maisha yao yote, na hao watumishi wanakuwa ni mali ya hao mabibi na mamlaka ya kuwafanya lolote ni juu yao.

Ibrahimu hakumuoa Hajiri bali alipewa, ikiwa na maana kuoa inatokana na matakwa ya mtu binafsi kutamani kuoa au kuchagua. Ila kupewa ni kitendo cha ridhaa ya mwingine kukushawishi

kufanya kitu fulani ambacho kinaweza kikawa chema au kibaya. Simaanishi kuwa Ibrahimu alizini, bali namaanisha kuwa tukae kwenye tafsiri halisi ya kile kilichofanyika kwa desturi za kale, nini tafsiri yake.

Desturi hii ya mabibi kutoa wajakazi wao, ilikuwa kawaida hata kwa mke wa Yakobo. Mwanzo 30:1.3 *Naye Raheli alipoona ya kuwa hamzalii Yakobo mwana, Raheli alimwonea ndugu yake wivu. Akamwambia Yakobo, Nipe wana; kama sivyo, nitakufa mimi. Yakobo akamghadhibikia Raheli, akasema, Je! Mimi ni badala ya Mungu, aliyekuzuilia uzao wa mimba?* ***Akasema, Yuko mjakazi wangu, Bilha, uingie kwake ili kwamba azae juu ya magoti yangu, nami nipate uzao kwa yeye.***

Kwa ujumla kwamba, hii desturi huwa haiitwi kuoa kwa wakati huo, ila ni kuazimwa mke na mtu anayemmiliki na akighaili anaweza kukunyang'anya au kumfukuza na sheria hii iliheshimika kwa wakati huo. Kwa hiyo basi, uhalali wa huyo mjakazi kuwa mke daima na watoto wake inategemeana atakavyojinyenyekeza kwa bibi yake maisha yake yote. Rejea Mwanzo 16:9 *Malaika wa Bwana akamwambia**, Rudi kwa bibi yako, ukanyenyekee chini ya mikono yake***

Rejea maneno haya "***Rudi kwa bibi yako, ukanyenyekee chini ya mikono yake"***

Kauli hii ya Malaika inatumulikia mwanga mkubwa wa kuijua tabia ya Hajiri kwamba, alikosa unyenyekevu kwa bibi yake, ndio maana malaika alimwambia nenda ukanyenyekee kwa Bibi yako. Hivyo ni wazi kuwa malaika mwenyewe alibaini kuwa Hajiri alikosa unyenyekevu (alikuwa na kiburi) kwa Bibi yake. Na hii tabia ya kiburi iliendelea kuonekana kwa mwanae Ishmael, ukisoma Mwanzo 21:8.*9 Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya; Ibrahimu akafanya karamu kuu siku ile Isaka alipoachishwa kunyonya. Sara* ***akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka.*** *Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu,*

*Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka.*

Kulingana na desturi za wakati huo, nafasi ya kuwa mke kwa mume chini ya Bibi ambaye ndiye mke wa ndoa, iliendelea kuwepo kwa sharti la (aliyepewa mume wa kuazimwa) kuendelea kumuenzi na kumuheshimu Bibi aliyempatia mume. na iwapo hatozingatia hilo mara tu anapoteza uhalali wake wa kuwa mke kwa mume wa Bibi yake. Na iwapo atafukuzwa huyo mwanamke, mume haruhusiwi kamwe kumfuatilia tena kwa siri au kwa dhahiri ikiwa na maana kuendelea naye katika mahusiano ya mke na mume, isipokuwa mtoto anaweza kumtembelea baba yake nk.

2. **Vizazi vya Ishmael Mwana wa Ibrahimu kwa mjakazi ni hivi.**

   Mwanzo 25:13.16 *Na haya ndiyo majina ya wana wa Ishmaeli, kwa majina yao, na kwa vizazi vyao. Mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, ni Nebayothi, na Kedari, na Abdeeli, na Mibsamu, na Mishma, na Duma, na Masa, na Hadadi, na Tema, na Yeturi, na Nafishi, na Kedema. Hao ndio wana wa Ishmaeli, na hayo ni majina yao, katika miji yao, na katika vituo vyao, maseyidi kumi na wawili kwa kufuata jamaa zao.*

   ***Orodha kamili ya vizazi vya Ishmael mwana wa Ibrahimu kwa mujibu wa Biblia.***

   1. Nebayothi,
   2. na Kedari,
   3. Abdeeli, na
   4. na Mibsamu,
   5. na Mishma,
   6. na Duma
   7. na Masa,
   8. na Hadadi,
   9. na Tema,

10. na Yeturi,
11. na Nafishi,
12. na Kedema.

Linganisha na majina ya wana wa Ismail kwa mujibu wa historia ya Waislamu. Tazama Jeduali lifuatalo

| Na. | Nasaba ya Biblia Wana wa Ishmael | Na. | Nasaba ya Quran na Hadith za Waislam, Wana wa Ismail |
|---|---|---|---|
| 1 | Nebayothi, | 1 | Banalut |
| 2 | Kedari, | 2 | Adhail |
| 3 | Abdeeli, | 3 | Mubsham |
| 4 | Mibsamu, | 4 | Mishmaa |
| 5 | Mishma, | 5 | Dumana |
| 6 | Duma | 6 | Misha |
| 7 | Masa, | 7 | Hada |
| 8 | Hadadi, | 8 | Yitma |
| 9 | Tema, | 9 | Ytur |
| 10 | Yeturi, | 10 | Nafiys |
| 11 | Nafishi, | 11 | Qaidam |
| 12 | Kedema. | 12 | Qaidar |

3. **Tafsiri sahihi ya maana ya kizazi cha Ibrahimu.**
   Maana ya vizazi vya Ibrahimu, au sifa ya kuitwa watoto wa Ibrahimu au sifa za kuitwa ukoo wa Ibrahimu.

   a. Kuzaliwa na Ibrahimu. Iwapo mtu amezaliwa na Ibrahimu atakuwa na sifa za kuwa mwana wa Ibrahimu, lakini, ili kizazi cha aliyezaliwa na Ibrahimu kiendelee kuitwa kizazi cha Ibrahimu chenye sifa zote na vigezo, ni sharti
   b. Yeye mwenyewe ahakikishe anaoa miongoni mwa ndugu wa Kiebrania au kizazi cha Ibrahimu. Mwanzo 24.

Inaelezea maagizo ya Ibrahimu kuwa mwanawe Isaka asiposewe mke kutoka binti za Kanaani au wasiokuwa Waebrania, lengo ni kuhifadhi mbegu halisi ya Kiebrania bila kuchanganya, ikiwa na maana haikutakiwa ikatokea akazaliwa mtoto au watoto machotara.

**4. Maelezo ya ziada.**

a. Ishmail ni mwana wa Ibrahimu, lakini alizaliwa na asiyekuwa Mwebrania, ikiwa na maana ni mbegu mbili, Mmisri na Mwebrania Rejea Mwanzo 16.

b. Ishmael alioa, lakini alioa mwanamke wa Kimisri Soma Mwanzo 21:21. Ikiwa na maana tofauti na Isaka Mwanzo 24, kwamba alioa Mwebrania, ikiwa na maana Isaka aliendeleza kabila na asili ya baba yake Ibrahimu, lakini Ishmael hakuendeleza kabila wala asili ya baba yake Ibrahimu, isipokuwa aliendeleza kabila ya mama yake Mmisri. Kwa hiyo, kwa lugha rahisi kwamba, Ishmael alipoteza asili ya Ibrahimu.

c. Kizazi cha Ibrahimu kiliishia kwa Ishmael tu, baada ya hapo alikuwa anazaa na kuzaana na mataifa mengine na watu wa asili nyingine, na hivyo kilichoendelea katika koo za Ishmael sio ukoo au kabila ya Ibrahimu tena bali ni kinyume chake.

**Kwa mifano.**

-Kuna watu waliwahi kuniambia kwamba, asili ya Wadoe wa Pwani (Tanzania) eneo la Halmashauri mpya ya Chalinze ni Wanyamwezi. Inaaminika walikuja Pwani kuhemea, kisha waliwapenda Wang'hwele wakaoa na kuweka maisha kabisa huko Pwani, mwisho likatokea kabila chotara la Wang'hwele nalo ni Wadoe, ambao hata lugha yao ina utofauti fulani kataka matamshi na wenyeji wao.

Swali la kujiuliza ni kwamba, je hata kama ni kweli asili yao ilikuwa ni Wanyamwezi kule walikotokea, je hadi sasa ni Wanyamwezi au Wadoe?

*d.* **Watoto wa Ibrahimu wa imani.** Inawezekana mtu akawa mtoto wa Ibrahimu kwa imani iliyo sawa na Ibrahimu. Mwanzo 15:1.6. Hata hivyo maandiko yanasema kuwa mwana wa Ibrahimu kwa imani anapaswa kutenda matendo ya Ibrahimu kwa imani sio maneno tu Mathayo 3:9. Baraka ya Ibrahimu Mwanzo 12:1.4, Baraka ya Ibrahimu ilifuata kizazi kwa kizazi katika uzao halali wa Ibrahimu, nikiwa na maana ni ule uliokuwa ukizaana kupitia ndugu kwa ndugu Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Israel wote, Yesu. Kutoka 3:6 *Tena akasema,* ***Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo****.* Ikiwa na maana Mungu anaonyesha nasaba halisi ya wana wa Ibrahimu wenye kuwakilisha Baraka ya Ibrahimu au wenye kuwakilisha Imani sahihi ya Ibrahimu. Mwisho wa yote Ibrahimu anawakilishwa na mtu mmoja tu ambaye ni Yesu, ndiye anayewakilisha agano la Ibrahimu na Mungu. Wagalatia 3:*14 ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.* Matendo ya Mitume 4:12.

*e.* **Sayansi ya uhifadhi wa mbegu za mimea.** Kwa kawaida katika kanuni ya kitaalamu ya kuhifadhi mbegu za mimea, huwa inatakiwa kila mbegu itengwe isichanganyike na mbegu nyingine, kwani kuna uwezekano mbegu mojawapo ikapotea au ukashindwa kutofautisha. Inashauriwa kila mbegu ipandwe eneo lake maalumu kwa kuwa kila mbegu inatabia maalumu isiyokubaliana na mbegu nyinge. Tendo la kuchanganya mbegu ni tishio la kupoteza au kuharibu mbegu.

5. Mila ya Ibrahimu. Moja ya mila madhubuti ya Ibrahimu ilikuwa ni kutunza asili ya kizazi chake kisiwe chotara. Mwanzo 24. Ibrahimu aliwausia wanawe kwamba wasichanganyane na watu wa mataifa au makabila mengine katika kuoa na kuzaana, na wana wa Ibrahimu wote kizazi chao walizingatia hilo na wale baadhi ya waliofanya kinyume walikalipiwa sana hata kulazimishwa kuwaacha wake zao ambao wasio wa Kiebrania, tusome Nehemia 10:29.30 *wakaambatana na ndugu zao, wakuu wao, nao wakaingia katika laana na kiapo, ya kuwa wataiendea torati ya Mungu, iliyotolewa kwa mkono wa Musa, mtumishi wa Mungu, na kuziangalia, na kuzitenda, amri zote za Bwana, Bwana wetu, na hukumu zake na sheria zake;* ***wala tusiwaoze watu wa nchi binti zetu, wala kuwatwalia wana wetu binti zao;***

## II. KATI YA ISHMAEL NA ISAKA YUPI ALIYEPATA HAKI YA MZALIWA WA KWANZA KWA IBRAHIMU.

Kwa mujibu wa mijadala mingi, na wasomi wengi wa maandiko matakatifu na vitabu mbalimbali, mara nyingi kuna wanaosema kuwa Ishmael ndiye mzaliwa wa kwanza wa Ibrahimu na pia alipata haki ya mzaliwa wa kwanza. Na kuna wanaosema kuwa mzaliwa kwanza aliyetambulika alikuwa Ishmael. Nini ukweli wa hilo?

Kwa mujibu wa historia na taratibu za kimaandiko na mila na desturi za mababu wa imani inaonyesha kwamba haki ya mzaliwa wa kwanza inaweza kutolewa kwa kanuni kuu mbili, kwa wakati wa imani ya kipindi cha Ibrahimu na kwa wakati wa sheria yaani kipindi cha Musa.

## A. Kipindi cha Ibrahimu na mababa wa imini, Isaka, Yakobo.

Haki ya mzaliwa wa kwanza ilitolewa kwa misingi mikuu miwili

1. Mzaliwa wa kwanza wa namba. Ninaposema mzaliwa wa kwanza wa namba ninamaanisha ni mzaliwa wa kwanza wa kutangulia kuzaliwa. Aina hii ya uzaliwa wa kwanza, unajulikana kama ni uzaliwa wa kwanza wa namba. Ikiwa na maana wa kwanza, wa pili, watatu nk. Katika mfuatano huo ndiyo tunapata mzaliwa wa kwanza kulingana na namba iliyo anza. Mwanzo 16: *Hajiri akamzalia Abramu mwana wa kiume; Abramu akamwita jina lake Ishmaeli, yule mwanawe, ambaye Hajiri alimzaa.*

   Kwa wakati ule Ishmael ndiye aliyejulikana na kuaminika kuwa ndiye mwana wa kwanza wa Ibrahimu, na ilichukua muda mrefu zaidi bila ya Ibrahimu kupata mtoto mwingine, si kwa Hajiri wala kwa Sara.

   Mwanzo 17:15.*19 Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara. Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake. Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa? Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake.*

Kauli ya Ibrahimu kumtetea Ishmael abaki kuwa mzaliwa wa pekee wa Ibrahimu, linaonyesha wazi kuwa Ishmael alikuwa ndiye mzaliwa wa kwanza wa namba, lakini Mungu hakuridhia mzaliwa kwanza wa namba kuwa mzaliwa wa kwanza wa haki ya kurithi kwa Ibrahimu. Ninakusudia kwamba, alikuwa mzaliwa wa kwanza wa namba, lakini hakuwa mzaliwa wa kwanza wa haki ya kurithi.

Kauli ya Sara ya kukataa Ishmael asiwe mrithi pamoja na mwanawe Isaka katika kitabu cha Mwanzo 21:9.10, haikuwa ni husuda (wivu) bali ilikuwa haki na mpango wa Mungu kwani Mungu alitangulia kuzungumza na Ibrahimu katika Biblia kitabu cha Mwanzo 17:15.19 kuwa Ishmael hatakuwa mrithi wake kama mzaliwa wa kwanza. Ibrahimu alionyesha wazi kuwa kama ingelikuwa ni mapenzi yake, asingelipenda Ishmael aondolewe katika nafasi ya mrithi wa Ibrahimu, hili aliliongea wazi mbele za Mungu soma Mwanzo 17:17.19, bali Mungu alimwambia kwa msisitizo kwamba, Sara atazaa mwana ambaye huyo ndiye mrithi halali wa Ibrahimu na ndiye mzaliwa wa kwanza wa haki wa Ibrahimu.

Watu wengi wanamchukulia vibaya Sara kuhusu tendo lake la kumfukuza Hajiri na Ishmael, huku wakihusisha hatua yake ya kumfukuza Hajiri na Ishmael kama ni wivu au chuki kwa mke mwenza, lakini kiuhalisi Ibrahimu Alishaelezwa wazi na Mungu kwenye Mwanzo 17:15.19, kuwa Ishmael hatakuwa mrithi wake kamwe bali yule atakayezaliwa kwa mke wake ambaye Mungu aliweka ahadi kuwa, kwa mke wake wa kwanza ambaye ndiye mke wa ujana wake waliopitia magumu yote katika utumishi, atampatia uzao utakaomrithi, wala hajaahidi kumpatia mwana kwa mjakazi kisha awe mrithi, rejea Mwanzo 17:15.19, tendo la kukataa urithi mbadala au wa njia ya mkato ulifikiriwa mara nyingi na Ibrahimu (kumrithisha mfanyakazi wake kwakuwa hana mwana) Mwanzo 15:1.6 lakini Mungu mara zote alimuasa

Ibrahimu kuwa Mungu hahitaji kusaidiwa kutatua tatizo kwa njia ya mkato kwa kuwa ameona kama amekawia na kwa udhaifu wake wa kibinadamu akakata tamaa na kuamua akatishe. Rejea Mwanzo 18:13.14. Katika andiko hilo la Mwanzo 18:13.14 inathibitisha kuwa, Mungu kwake hakuna jambo gumu, ikiwa na maana Ibrahimu na Sara walianguka kutoka katika imani ya kumuamini Mungu kuwa angewapatia mtoto, hii ni kulingana na jitihada zao za muda mrefu kuonekana kugonga mwamba. Hili lilikuwa kosa la upungufu wa imani kwa wanadamu wote huwa tuna mwisho wetu wa kuvumilia, ikipita kaisi cha kawaida wengi tunakata tamaa.

**Maamuzi ya Mungu mwenye haki**

Kukataa Ishmael asiwe mrithi wa Ibrahimu, haya yanadhihirisha wazi kuwa, ni maamuzi ya Mungu mwenye haki. Hebu ungejaribu kufikiria hata kibinaadamu, Sara aishi na Ibrahimu miaka 90 kisha asizae, na Mungu amuache Sara na mwanawe na kumpa Ishmael mwana wa mjakazi awe mrithi wa Ibrahimu. Ni wazi halijakaa vizuri jambo hilo, na Mungu angepoteza sifa zake za kuwa Mungu mwenye haki. Lakini pia walimwengu wengi wangekata tamaa kwa kumtumaini Mungu na kusubiri kisha huyo Mungu kuwaacha na kuwafanyia vitu tofauti na matarajio yao, kwa wale waliomuamini na kumsubiri. Mungu kumpa Sara mtoto ni kulitetea jina lake na kuonyesha uaminifu wake. Zaburi 119:90 *Ee Bwana, neno lako lasimama Imara mbinguni hata milele. Uaminifu wako upo kizazi baada ya kizazi, Umeiweka nchi, nayo inakaa.*

**Angalia kwa makini yafuatayo**

a. Ombi la Ibrahimu tangu mwanzo ni kupata mrithi soma Mwanzo 15:1.6.
b. Mungu alielekeza kuwa mrithi ni Isaka. Angalia Mwanzo 17:15.19.

c. Ibrahimu alimrithisha yote mwanawe Isaka na kuwaondoa watoto wa wakeze wengine mahali alipoishi Isaka Mwanzo 25:5.6 *Ibrahimu akampa Isaka yote aliyokuwa nayo. Lakini wana wa masuria aliokuwa nao Ibrahimu, Ibrahimu akawapa zawadi, naye akawaondoa katika mahali alipokaa Isaka mwanawe, wakati wa uhai wake, waende pande za mashariki, mpaka nchi ya Kedemu.*

**Kupokonywa haki ya uzaliwa wa kwanza au kuipoteza.**

Katika zamani hizo, haki ya uzaliwa wa kwanza haikuzingatiwa kwa namba pekee, ila kwa kukubalika. Au kuwa na sifa za kuwa mzaliwa wa kwanza, kwa mfano unaweza kupoteza haki ya uzaliwa wa kwanza wa namba iwapo utafanya jambo baya la kuchukiza, baba anaweza kuiondoa haki yako ya kuwa mzaliwa wa kwanza na kumpa amtakaye Mwanzo 49:1.*4 Yakobo akawaita wanawe, akasema, Kusanyikeni, ili niwaambie yatakayowapata siku za mwisho. Kusanyikeni, msikie, enyi wana wa Yakobo, Msikilizeni Israeli, baba yenu.* ***Reubeni, u mzaliwa wangu wa kwanza, Nguvu zangu, na malimbuko ya uwezo wangu. Umewapita wengine kwa ukuu na kwa nguvu. Umeruka mpaka kama maji, basi usiwe na ukuu, Kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako, Ukakitia unajisi; alikipandia kitanda changu.***

Yakobo alimyang'anya haki ya uzaliwa wa kwanza wa haki (Kukubalika), kwamba Reubeni hatakuwa mzaliwa wa mwenye haki ya ukuu na kumiliki katika Baraka na utukufu wa baba yake, bali alibakishiwa uzaliwa wa kwanza wa namba.

Mwanzo 48:17.20 *Yusufu alipoona kwamba babaye anaweka mkono wake wa kuume juu ya kichwa cha Efraimu, ikawa vibaya machoni pake. Akauinua mkono wa babaye auondoe katika kichwa cha Efraimu, ili auweke juu ya kichwa cha Manase. Yusufu akamwambia babaye, Sivyo, babangu, maana huyu ni mzaliwa wa kwanza; weka mkono wako wa kuume kichwani pake. Babaye akakataa, akasema, Najua, mwanangu najua, yeye naye atakuwa taifa, yeye naye atakuwa mkuu; lakini ndugu yake mdogo atakuwa mkubwa kuliko yeye, na uzao wake watakuwa wingi wa mataifa. Akawabariki siku ile akasema, Katika ninyi Waisraeli watabariki, wakisema, Mungu na akufanye kama Efraimu na Manase. Akamweka Efraimu mbele ya Manase.*

Kwa ujumla nimekazia kwamba, tafsiri ya mzaliwa wa kwanza kwa mujibu wa maandiko hasa katika kipindi kabla ya sheria za Musa haikuwa kwa namba bali kwa haki.

Waliopoteza haki za uzaliwa wa kwanza ni wengi, lakini pia yupo mmojawapo aitwaye Esau Mwanzo 25:20.34

Kwa hiyo Ishmael kupoteza haki ya mzaliwa wa kwanza sio yeye peke yake.

2. Mzaliwa kwa kwanza wa haki. Ni Yule ambaye inaweza ikawa ni chaguo la Mungu tazama Mwazo 17:15.19. Au mzaliwa wa kwanza wa sifa zinazokubalika kuwa mzaliwa wa kwanza. Rejea Mwanzo 49:3.5. Mwanzo 48:21.22

**B. Mzaliwa wa kwanza kipindi cha sheria wakati wa Musa**
Katika kipindi hiki sheria ilitafsiri haki ya mzaliwa wa kwanza wa namba ndiye mwenye haki ya kuwa mrithi. Kumbukumbu la Torati 21:17. Kwa ujumla katika Torati imepambanuliwa sana nafasi ya mzaliwa wa kwanza jinsi

gani Mungu anavyowatazama. Lakini jambo la kuzingatia, Mungu pia anafanya yote kwa makusudi yake, Mungu hafungwi na sheria kutimiza matakwa yake. Kwa ujumla kilichofanyika kipindi cha Ibrahim, Isaka, na Yakobo ni maamuzi yaliyoongozwa na imani, na sio imani tu, bali pia Mungu aliwaongoza kufanya maamuzi sahihi juu ya msuala fulani kulinga na kusudi lake juu ya jambo hilo.

### III. Kulikoni Hajiri kutokuzaa tena na Ibrahimu kwa zaidi ya miaka 19?

Kwa mujibu wa maandiko matakatifu Biblia, kwamba, baada ya Hajiri kumzalia mtoto Ibrahimu, aliendelea kuishi kwenye familia ya Ibrahimu kwa zaidi ya miaka 13 Kabla ya kufukuzwa.

Mwanzo 17:23.25 *Ibrahimu akamtwaa Ishmaeli mwanawe, na wote waliozaliwa nyumbani mwake, na wote walionunuliwa kwa fedha yake, wanaume wote wa watu wa nyumba ya Ibrahimu, akawatahiri nyama ya magovi yao siku ile ile, kama Mungu alivyomwambia. Naye Ibrahimu alikuwa mwenye umri wa miaka tisini na kenda alipotahiriwa nyama ya govi lake.* ***Na Ishmaeli mwanawe alikuwa mtu wa miaka kumi na mitatu,*** *alipotahiriwa nyama ya govi lake.*

Kwa mujibu wa Mwanzo 17:23.25 kwamba, baada ya Hajiri kumzalia Ibrahimu, aliendelea na maisha katika familia ya Ibrahimu. Na hapa kuna swali au maswali kadha ya kujiuliza kwa kitendwili hiki. Kwani inaaminika Ishmael alitahiliwa akiwa na umri wa mika 13 sawa na Mwanzo 17:23.25. Na Hajiri alifukuzwa baada ya miaka kadha ya kuzaliwa Isaka, inakadiliwa baada ya miaka 4 au 5 au zaidi baada ya kutahiliwa Ishamael, hivyo inawezekana Ishmael alikuwa na miaka kati ya 17 au 19. Na ndio maana maandiko yanamtaja kama kijana Mwanzo 21:*14 Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba.*

Kwa maelezo zaidi kuhusu umri wa Ishmael fuata link

https://amazingbibletimeline.com/blog/old-ishmael-abraham-sent-away/

maswali ya msingi.

1. Iweje Hajiri hakumzalia tena Ibrahim kwa zaidi ya miaka 19 kama alikuwa mkewe?
2. Je Hajiri baada ya kumzaa Ishmael na yeye akawa tasa?
3. Je Ibrahimu na Hajiri walitengana mara tu baada ya kumzalia mtoto mmoja?
4. Au Ibrahimu kupewa Hajiri kumuingilia haikuwa na dhamira kuwa mkewe moja kwa moja, bali ilikuwa kwa lengo la kutafuta mtoto, na baada ya kukipata mtoto ndio imekuwa mwisho mahusiano?

Haya ni maswali ambayo yanahitaji majibu ya ufasaha, lakini kati hayo inawezekana mojawapo likawa ndio jibu sahihi.

### IV. Hajiri na Ishmael walikimbilia wapi, na alioa wapi, na kizazi chake Ishmael kiliishi maeneo au nchi ipi.

**Tuna kusudia kuichimba historia ya Muhammad.** Nadhani ni jambo la muhimu sana, kuiangalia nasaba yake kwa kina, lakini ni vema kuifuatilia familia inayodaiwa kuwa ndio chimbuko la kuzaliwa kwake au kutokea kwake Muhammad humo.

Ni jambo la kawaida kusikia wana zuoni wa Kiislamu kuelezea hili la Muhammad kutokea kwenye nasaba ya Ibrahimu kupitia Ishmael, ambaye inadaiwa kuwa aliishi Makka Saud Arabia, na kujenga msikiti, na kuhusishwa na baadhi ya matukufu ya Makka, kama vile Msikiti wa Makka, maji ya Zamzam, na vilima vya Safa na Marwa kwamba ndio eneo ambalo Hajiri alipoishiwa maji na kukimbia baina ya vilima hivyo viwili vya Saafa na Marwa. Ukweli wa hili nakuahidi kuwa utajulika kweupe kabisa. Kama vile kitabu

chetu kinavyoitwa **Historia Halisi ya Maisha ya Mtume Muhammad**, basi tegemea kila kitu kukipata wazi na kwa ushahidi usiokuwa na kigugumizi chochote.

### A. Je! Hajiri aliachwa kama mke au alifukuzwa kama adui?

Kwa mujibu wa Biblia Hajiri hakuachwa kama mke vile anavyoachwa, kupewa talaka au kupewa utaratibu wa kisheria katika kuachwa kwake, bali alifukuzwa yeye na mwanawe. Soma

Mwanzo 21:11.14 *Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa. Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyu naye ni uzao wako.* ***Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba.***

Hii ndio hali aliyoondoka nayo Hajiri nyumbani kwa Ibrahimu. Kwamba alifukuzwa kwa sababu ya tabia za dharau kubwa kwa bibi yake ambaye kwa wema wake alimpatia Hajiri mume wake. Sara alitegemea Hajiri angemuheshimu zaidi bosi wake Sara, na kuthamini tendo kubwa na ngumu la mjakazi kupewa mume wa bibi yake, lakini ikawa kinyume chake. Kukatokea kiburi jeuri dharau nk. Haikuishia hapoo, pia hiyo tabia ikatokea kwa mwanawe Ishmael kuonyesha dharau za wazi. Kiuhalisia familia ya Ibrahimu ilijikuta katikati ya machafuko ya kifamilia mara tu ya Hajiri kupata nafasi kwa Ibrahimu.

Rejea. Mwanzo 16:*4.5 Basi akamwingilia Hajiri, naye akapata mimba. Naye alipoona ya kwamba amepata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake. Sarai akamwambia Abramu, Ubaya ulionipata na uwe juu yako; nimekupa mjakazi wangu kifuani mwako, naye alipoona kwamba amepata mimba, mimi nimekuwa duni machoni pake. Bwana na ahukumu kati ya mimi na wewe.*

Kwa ujumla, maelezo ya Sara yalikuwa wazi, na Ibrahimu hajayakanusha kusema Sara ni mwongo, unamzushia mjakazi wako, bali alisema kwamba, maamuzi juu ya majakazi yapo kwa Sara mwenyewe kwani mjakazi ni wa kwake mwenyewe.

Rejea nyingie.

Mwanzo 16:*8.9 Akamwambia, Hajiri, wewe mjakazi wa Sarai, unatoka wapi, nawe unakwenda wapi? Akanena, Nakimbia mimi kutoka mbele ya bibi yangu Sarai.* ***Malaika wa Bwana akamwambia, Rudi kwa bibi yako, ukanyenyekee chini ya mikono yake****.*

Mwanzo 21:9.10 *Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu,* ***anafanya dhihaka****. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka.*

Ni wazi unaweza kutathmini hali halisi ya maisha ilivyobadilika mara tu Hajiri alipopewa nafasi ya kuwa mke kwa Ibrahimu na kuzaa mtoto mmoja. Hali ilikuwa haivumiliki kwa ujumla wake. Watu wengi wanadhani Sara alikuwa na wivu, lakini si kweli bali nidhamu ilikosekana kabisa katika familia ya Ibrahimu, kiburi kilishika hatamu yake. Kwa ujumla hali ilikuwa ni tete.

Hii ndio iliyopelekea Hajiri kufukuzwa badala ya kuondoka kwa heshima. Tendo la kufukuzwa linatokana na kukosekana kwa ustaarabu kwa Hajiri na Ishmael. Ni wazi Sara alijutia maamuzi yake ya kujaribu kutafuta njia ya mkato ili apate mtoto haraka

haraka kumbe ndio amefungulia mlango wa kuivuruga ndoa yake na familia kwa ujumla.

**B. Hajiri na Ishmael waliekea wapi mara ya baada ya kufukuzwa.**

Mwanzo 21:14 *Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika* ***jangwa la Beer-sheba.***

Maandiko yanasema alipotelea katika Jangwa la Beer Sheba. Katika kupata hakika kuhusu eneo ambalo Ishmael na wanawe waliishi na mataifa yao na koo zao, ili usisumbuke, mambo ya kuzingatia ni kwanza rejea Mwanzo 21:14 baada ya kfukuzwa alielekea wapi. Jambo la pili rejea utabiri wa Malaika ulivyosema wapi makazi ya Ishmael na vizazi vyake wataishi. Rejea Mwanzo 16:12 *Naye atakuwa kama punda-mwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake,* ***naye atakaa mbele yao ndugu zake wote.***

Mambo ya kuzingatia ni haya.

1. Alipofukuzwa alielekea wapi? Jibu, aliekea jagwa la Beersheba. Huko mbele tutaiangalia Beersheba ilipo
2. Utabiri wa Malaika kuhusu Ishmael kwamba alitabiriwa ataishi wapi na kizazi chake. Hili nalo ni jambo la muhimu sana, ambalo litasaidia kuondoa utata wote.
3. Wapi Ishmael alioa, au nchi gani ambapo Ishmael aliweza kuoa mke wake?


**Maelezo kwa kina:**

1. Mara baada ya Hajiri na Ishmael kufukuzwa waliekea jagwa la Beersheba. Beersheba ipo kaskazini mwa Israel (Kanaani) inaaminika kwamba hata kisima alichokiona Hajiri

hakikuwa Makka bali kipo maeneo ya Beersheba jirani na Israel Jangwa la Parani.

Kisima alichokiona Hajiri kamwe hakikuwa Makka Saudi Arabia. Hili ni jambo la kushangaza sana, kwa mujibu wa Quran na Hadithi za Kiislamu kudai kuwa Saafa na Marwa iliyopo Makka ndipo Hajiri alipokuwa akikimbia kwa kutafuta maji, lakini ukweli wa kijografia unabainisha hilo sio la kweli kabisa kwa asilimia zaidi ya mia moja, kwa ushahidi huu unaothibitisha vilima vya Saafa na Marwa pamoja na maji ya Zamzam ya huko Makka hayana uhusiano na Historia ya Hajiri na Ishmael wala Ibrahimu, ni kwa ushahidi ufuatao.

## a. Beersheba ipo wapi. Tazama ramani.



Kwa mujibu wa ramani ya hapo juu, tunaiona mishale inaonyesha maeneo muhimu, lakini pia inaonyesha Ibrahimu alikuwa anaishi eneo lililokuwa linaitwa **Gerar Kusini mwa Kanaani au Israel** Mwanzo 20:1, kwa Waameleke rejea Mwanzo 21:22.34. mwendo mfupi unafika Beersheba ambapo Ibrahimu aliapiana na mfalme wa Waameleki na kupanda mti wa mkwaju rejea Mwanzo 21:22.34. Na mwendo mfupi kufika eneo ambalo Hajiri alipoishiwa maji ambapo ukiangalia ramani yetu hapo juu utaona mahali panaitwa Jangwa la Beer Sheba (Wilderness of BeerSheba) Kusini Magharibi mwa Israel njia ya kuelekea Misri katika Jangwa la Shur kwa Sasa ipo kwenye nchi inayopakana na Israel kwa Kusini ambayo ni Jordan


KISIMA CHA HAJIRI ALICHOJIONA ALIPOKIMBIA HAKIPO MAKKA

Mara kadha Waislamu wansisitiza sana, kwamba kisima hicho kipo Makka, lakini pia kuna wengine wanaodai kuwa Waisrael walipitia Makka kwenda Israel walipotoka utumwani Misri. Ki uhalisia kwamba kwa mujibu wa Jografia ya zamani watu wa Makka hawakuweza kwenda Shamu isipokuwa sharti wapitie Midiani (Madina) Hadi jirani na Jordani kuelekea Moabu na ndipo waingie Shamu (Syria)

Tazama Ramani ifuatayo utaona Makka ilipo, kisha utanona ili waende Shamu Syria utaona lazima wapite Madina, hakuna njia ya mkato isipokuwa ni hiyo tu. Magharibi mwa Makka kuna bahari ya Red Sea na kwa wastani Saudi Arabia imezunguukwa na bahari magharibi, kusini, Mashariki kote ni bahari isipokuwa upande wa kaskazini mwa Saudi Arabia pekee ndio hakuna bahari.




Ramani yetu inayofuata itaonyesha mipaka ya zamani ya mataifa ambayo ni ndugu wa Israel.


0 (km) 20
Byblos
Beirut
Sidon
Tyre
SIZU
ASSYRIAN EMPIRE
Damascus
PHOENICIAN
STATES
Acre
KINGDOM OF
ARAM DAMASCUS
NAHOR
ABRAM'S
BROTHER
Umomium
Mediterranean
Sea
KINGDOM OF
ISRAEL
Samaria
ARAMEAN
TRIBES
Shechem
Jerash
Jaffa
KINGDOM OF
AMMON
Beit El
Rabbath-Ammon
Jericho
Jerusalem
Ashdod
Lachish
LOT
Ashkelon
Dibon
Hebron
KINGDOM OF
JUDAH
Gaza
KINGDOM OF
MOAB
Beersheba
KATURA'S
SON
ARABU
TRIBES
ESAU
NABATU TRIBES
KINGDOM OF EDOM
ISHMAEL
Petra
MIDIANITES

Baada ya miaka mingi lile jangwa alilokimbilia Hajiri la Beersheb waliishi Wana wa Esau yaani Edom ***(Kwenye ramani utanona – Esau Kingdom of Edom)*** ni mtoto wa Isaka mkubwa aliyepoteza uzaliwa wake wa kwanza kisha akauchukua Yakobo na pia wana wa Lutu ***(Lutu ni ndugu yake Ibrahimu rejea Mwanzo 12:4 na Mwanzo 19:36.38)*** ambao ni Moabu ambayo nchi hiyo sasa inaitwa Jordan. Kwa wastani Saudi Arabia haijapakana na nchi ya Israel kiasi kwamba kwa hali ya kawaida mtu aweze kutembea kwa miguu na kufika mara moja, ikiwa na maana tunajaribu kuiangalia dhana inayodai kuwa Hajiri na Ishmael walikimbilia Makka na ndipo walipoona kisima cha maji karibu na vilima viwili vya Saafa na Marwa.

**Umbali kutoka Yerusalemu hadi Saudi Arabia (Makka).**

Umbali kutoka Kanaani hadi Saudi Arabia katika mji wa Madina ni wastani wa kilomita 1238. Kutoka Madina kwenda Saudi Arabia masaa 5 na dakika 15 (491.2 km) kwa njia ya kawaida (kwa gari).

Kwa hiyo tunaona umbali kati ya Kanaani na Makka, ni sehemu ambayo sio rahisi kufika kwa miguu kwa muda mfupi, zaidi ya kilometa 1800 ni wastani wa Kutoka Dar es salaam kwenda Bukoka kilometa 1378 kwa basi inachukua masaa 17 na dakika 48. Ni wazi Hajiri asingeliweza kutembea umbali huo kwa siku chache.

Kwa wastani taarifa za kihistoria na za Quran kudai kuwa Makka ndipo mahali alipofikia Ishmael na ndipo alipoishiwa maji, kwa hakika hazina uwiano kabisa na ukweli wa Jografia na uwiano wa maandiko ya vitabu vingine vya kale kama Tenakh (kitabu cha Wayahudi) na Biblia. Kwa wastani na hata Quran yenyewe inapingana yenyewe kwa yenyewe ukiangalia maelezo Baqarah 2:125.127 na Quran 34:44.

Quran Surat Al baqarah **125.** Na kumbukeni tulipo ifanya ile Nyumba (ya Alkaaba) iwe pahala pa kukusanyikia watu na pahala

pa amani. Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia. Na tuliagana na Ibrahim na Ismail: Itakaseni Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu na wanao jitenga huko kwa ibada, na wanao inama na kusujudu

---

وَإِذۡ قَالَ إِبۡرَٰهِـۧمُ رَبِّ ٱجۡعَلۡ هَٰذَا بَلَدًا ءَامِنٗا وَٱرۡزُقۡ أَهۡلَهُۥ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ
مَنۡ ءَامَنَ مِنۡهُم بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِۚ قَالَ وَمَن كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُۥ قَلِيلٗا ثُمَّ
أَضۡطَرُّهُۥٓ إِلَىٰ عَذَابِ ٱلنَّارِۖ وَبِئۡسَ ٱلۡمَصِيرُ ١٢٦

**126.** Na alipo sema Ibrahim: Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.

---

وَإِذۡ يَرۡفَعُ إِبۡرَٰهِـۧمُ ٱلۡقَوَاعِدَ مِنَ ٱلۡبَيۡتِ وَإِسۡمَٰعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ
أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ١٢٧

**127.** Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi.

رَبَّنَا وَٱجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا
وَتُبْ عَلَيْنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾

**128.** Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma ulio silimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.


**Maelezo.** Ukiambatanisha sura hiii na aya zake, na ukilinganisha na wanazuoni wasemavyo kuhusu muktadha wake au maana yake au makusudio yake. Inaonyesha kwamba Makka ni sehemu ambayo Ibrahimu aliwahi kuishi, ndipo Ishmael na mama yake walipofikia na wakaishiwa maji. Hapo kuna kumbukumbu 1. Vilima viwili Saafa na Marwa 2. Nyumba ya Msikiti wa Makka. 3. Kisima cha maji ya Zamzam ambacho pia umbali wake kutoka Makka hadi Zamzama ni wastani wa mwendo mfupi kabisa unaweza kutembea kwa miguu kufika kwenye kisima.

Lakini bado Quran hiyo hiyo inakanusha ujio wa nabii yoyote Makka kabla ya Muhammad, ikiwa na maana katika mji wa Makka hajawahi kwenda nabii yoyote, wala hawajawahi kupelekewa vitabu wavisome Quran Sabaa (34) 44. Ni wazi aya hii inaungana na ukweli wa Kijografia kwamba hajawahi kwenda huko Ibrahimu wala Hajiri wala Ishmael. Kwa nini? Ni kwa sababu ya umbali wa kutoka Kanaani hadi Makka, lakini pia hakuna vitabu vingine vya zamani vinavyomuunga mkono Muhammadi kuhusu dai lake kupitia kitabu alichopewa.

### b. Ishmael alikimbilia na kuishi katika Jagwa la Shuri.

Kwa mujibu wa ushahidi wa kimaandiko na histori kwamba, Ishmael alikimbilia katika Jagwa la Shuri jirani na mpaka wa nchi ya Kanaani kwa wakati huo, lakini ni kwa sasa imepakana na Jordan.

**Tazama ramani ifuatayo.**




Maandiko yanaelekeza wapi wana wa Ishmael waliishi tazama Mwanzo 25:18 *Wakakaa toka* ***Havila mpaka Shuri, unaoelekea Misri, kwa njia ya kwenda Ashuru****. Akakaa katikati ya ndugu zake wote.*

Ukiangalia kwa chini ya hii ramani, tunaisoma ni Kusini mwa Palestina au Kanaani, ambayo ni Israel ya sasa. Chini ya neno Israel kuna Shur kulia Jordan – Ammon. Kwa hiyo basi inaonyesha wazi kuwa Ishmael na Hajiri walikimbilia eneo hilo la Shur, ukiangalia

Jografia ya Mashariki ya Kati, Shuri ni mji jirani na Misri na ndio maana ilikuwa rahisi Hajiri kwenda kumuolewa mwanawe mke katika nchi ya Misri. Hili linakubalika kulingana na ujirani wa Shur na Misri. Lakini kwa mujibu wa Jiografia Shur ilikuwa ni jangwa kubwa linalotoka magharibi kwenda mashariki ambayo ni Assyria Iraq na Havila – Kuwait. Tazama ramani na mishale ya hapo juu.

Kwa ujumla historia haiwezi kudanganya hata kidogo. Kinachotakiwa ni kupata vielelezo sahihi vya kihistoria. Hivyo iwapo vitaangaliwa vielelzo hivyo, itabainika ukweli usiohitaji kupigiwa chapuo, wa wapi Ishmael na Hajiri walikimbilia na kuishi. Kwa kufanya hadithi iwe fupi, Hajiri na Ishmael hawakukimbilia Makka, licha ya Makka, lakini hata Madina hawakufika katika kukimbia kwao hata kuishi kwao. Kwa ujumla taarifa za Quran na za Muhammad zitatuingiza kwenye kuwaza mengi na kutafiti mengi ili kujua ilikuwaje kutoa taarifa ambazo tunashindwa kuzithibisha kwa mujibu wa mazingira yetu. Na kinachotutatiza zaidi, ni msimamo wa Waislamu kuhusu Quran kudai kwamba haina shaka hata kidoho na hakuna makosa hata kidogo. Sasa tunapoyaona haya bila yashaka wao ndio wanapaswa kujibu maswali haya.

### c. Utabiri wa Malaika wa eneo ambalo wapi Ishmael ataishi.

Mwanzo 16:11.12 *Malaika wa Bwana akamwambia, Tazama! Wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ishmaeli, maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako. Naye atakuwa kama punda-mwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake,* ***naye atakaa mbele yao ndugu zake wote.***

Rejea maneno haya “***naye atakaa mbele yao ndugu zake wote.”***

Kwa mujibu wa Biblia, ilitabiriwa wapi Ishmael ataishi, na aina gani ya maisha atakayoishi yeye Ishmael na kizazi chake, mataifa yao na idadi ya watoto na wakuu wao. Naomba unifuate kwa makini sana.

**Mambo yaliyoelezewa wazi yamuhusuyo Ishmael na kizazi chake.**

1. Hatakuwa na huduma ya kidini (agano) bali atakuwa mtu aliyefanikiwa (barikiwa) kuwa taifa kubwa. Mwanzo 17:18.19 *Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami* ***nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele*** *kwa ajili ya uzao wake baada yake.*

   Mwanzo 17:20.21 *Na kwa habari za Ishmaeli nimekusikia,* ***nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu.*** *Bali agano langu nitalifanya imara kwa Isaka, ambaye Sara atakuzalia majira kama haya mwaka ujao.*

   **<u>Tazama maneno haya kwa makini</u>**

   <u>Kwa Isaka</u> - ***nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele*** *kwa ajili ya uzao wake baada yake.*

   <u>Kwa Ishmael</u> - ***nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu***

   <u>Chunguza neno lililokosekana kwa Ishmael ni – Agano la Mungu.</u>

   Neno agano lina maana ya patano, lakini kwa wakati huo neno agano linawakilisha utawala wa kiroho au mwongozo wa kumuishia Mungu au dini. Kwa ujumla Isaka na kizazi chake walipewa usimamizi wa mambo ya kiroho au kidini. Kwa Ishmael hakuna ahadi ya kidini au kiroho.

2. Atazaa watoto 12. Ambao ni Maseyidi. Neno Maseyidi maana yake JUMBE. Au watawala wa koo 12 au mataifa 12. Cha kuzingatia ni nini Ishmael aliahidiwa. Ishmael aliahidiwa majumbe 12. Au kwa lugha nyingine, Ishmael aliahidiwa uongozi imara chini ya Majumbe 12. Katika lugha ya Kingereza neno Seyidi linatafsiri kama "Prince" Maseyid "Princes" Ikiwa na maana ya Wakuu 12. Au watawala 12. Kwa maelezo zaidi angalia kamusi, au soma Biblia ya Kingereza.

3. Maisha ya kustajabisha, ni kwamba, watu kwa kuona kana kwamba anafanya mambo mageni kwa jamii ikiwa na maana alifananishwa na punda mwitu. Punda mwitu akiwa mjini watu watamshangaa, na yeye atawashangaa watu. Halafu anaweza kuinua mkono wake juu ya watu, ikiwa na maana kuwapiga na wao watampiga, ikiwa na maana ni maisha ya piga nikupige. Rejea. Mwanzo 16:11.12 *Malaika wa Bwana akamwambia, Tazama! Wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ishmaeli, maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako. Naye atakuwa kama punda-mwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake,* ***naye atakaa mbele yao ndugu zake wote.***

   Mkono unatafsiriwa kama silaha, ama mamlaka ya kufanya jambo la kiutawala. Tafsiri ya utawala wa Ishmael na kizazi chake kwamba sio utawala imara wala kudumu, ndio maana inasema mkono wake utakuwa juu ya watu na mkono wa watu wote utakuwa juu yake. Hii inatafsiri maisha ya misukosuko.

4. Ataishi katikati ya ndugu zake. Ikiwa na maana makazi yake hayakuwa mbali na ndugu zake. Hii ina maana ndugu zake ni wenye nasaba ya Ibrahimu, Israel, Esau au Edom, Moabu

(watoto wa Lutu) Midiani ni mtoto wa Ibrahimu aliyemzaa na mwanamke mwingine baada ya kufariki Sara alimuoa Ketura ndiye aliyemzaa Midiani na Midiani ndiye aliyejenga mji au ndie mwenye nchi ya Midiani kwa wakati huo kabla ya Saudi Arabia kuhozi eneo lote la Jagwa na kuiita nchi moja ya Saudi Arabia.

Mwanzo 25:1.4 *Ibrahimu alioa mke mwingine jina lake akiitwa Ketura. Akamzalia Zimrani, na Yokshani, na Medani, na Midiani, na Ishbaki, na Sua. Yokshani akamzaa Sheba, na Dedani; na wana wa Dedani walikuwa Waashuri na Waletushi, na Waleumi. Na wana wa* ***Midiani*** *walikuwa, Efa, na Eferi, na Hanoki, na Abida, na Eldaa. Hao wote walikuwa ni wana wa Ketura.*

**Ni kina nani ambao walitambiriwa kuwa ndugu wa Ishmael ambao atakaa katikati yao? Ni hawa.**

1. Moabu na Amoni. Watoto na kizazi cha Lutu ndugu wa Ibrahimu. Rejea Mwanzo 12:4. Mwanzo 19:36.38

   Mwanzo 19:36.38 *Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao. Yule mkubwa akazaa mwana, akamwita jina lake* ***Moabu;*** *huyo ndiye baba wa* ***Wamoabi,*** *hata leo. Na yule mdogo naye akazaa mwana akamwita jina lake* ***Benami;*** *huyo ndiye baba wa* ***Waamoni hata leo.***

   Ndugu msomaji wangu, tunaona vile tunapoanza kuwatambua ndugu zake Ishmael na wapi makazi yao yalipo na wapi Ishmael atakuwepo kwa mujibu wa historia. Mbele tutaona ramani ili kuthibisha wapi hao wana wa Lutu waliishi hata leo.

2. Watoto wa Ibrahimu kwa mke mwingine aitwaye Ketura aliyemuoa mara tu alipofiwa na mkewe Sara.

Mwanzo 23:1.2 *Basi umri wake Sara ulikuwa miaka mia na ishirini na saba ndio umri wake Sara. Sara akafa katika Kiriath-arba, ndio Hebroni, katika nchi ya Kanaani. Ibrahimu akaja kumlilia Sara na kumwombolezea.*

Kwa mujibu wa Mwanzo 23:1.2 inathibitisha kuwa Ibrahimu alifiwa na mkewe Sara. Baada ya mazishi na maombolezo na kupita siku kadha wa kadha utaona kwenye sura inayofuata kwamba, Ibrahimu alioa mke mwingine aitwaye Ketura.

Swali la kujiuliza na hasa la kuwauliza ndugu zetu wapendwa Waislamu. Kwa nini Ibrahimu hakuenda kumchukua Hajiri baada ya Sara kufa?

***Ibrahimu Kuoa tena tazama***

Mwanzo 25:1.4 *Ibrahimu alioa mke mwingine jina lake akiitwa* ***Ketura.***

*Watoto aliozaa na Ketura baada ya kufariki kwa Sara*.

Mwanzo 25:2*. Akamzalia Zimrani, na Yokshani, na Medani, na* ***Midiani,*** *na Ishbaki, na Sua. Yokshani akamzaa Sheba, na Dedani; na wana wa Dedani walikuwa Waashuri na Waletushi, na Waleumi. Na wana wa Midiani walikuwa, Efa, na Eferi, na Hanoki, na Abida, na Eldaa. Hao wote walikuwa ni wana wa Ketura.*

Katika watoto wa Ketura mke wa Ibrahimu aliyemuoa baada ya kufariki Sara tunamuona Midiani. Mbaye pia amejenga mji uitwao Midiani (Madina) tutauona katika ramani. Lakini pia watoto wa Ketura walizunguuka eneo kubwa la Jangwa la Shur na Arabuni.

3. Watoto wa Israel yaani Yakobo mwana wa Isaka, mwana wa Ibrahimu. Ambao hao walipewa nchi yote ya Kanaani kwa amri ya Mungu mwenyewe. Kutoka 3:1.9. Mstari wa 8. Unasema.

*nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa* ***Mkanaani,*** *na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi.*

Tafsiri ya Mwanzo 16:11.12. Atakaa kati ya ndugu zake ni hii.

1. Wana wa Isaka – Israel Kaskazini mwa Ishmael.
2. Wana wa Ibrahimu kwa Ketura – Midiani – Kusini mwa Ishmael - Shur
3. Wana wa Lutu – Moabu – Amoni. Mashariki kaskazini mwa Ishmael.

Kwa ujumla Ishmael aliishi katikati ya ndugu zake sawa sawa na neno la Malaika Mwanzo 16:11.12. na Malaika hawezi kusema uongo.

**Wito kwa ndugu zetu Waislamu.**

Itazamwe kwa umakini Historia halisi ya mababa, kisha iamue kuhusu kipi ndio ukweli na kipi ni uongo. Kama Malaika alisema Ishmael ataishi katikati ya ndugu zake Mwanzo 16:11.12, hili la kutokomea hadi Makka kilometa zaidi ya 1800 kutoka Israel limetoka wapi na kasema nani? Kwa ujumla Uislamu utakuwa na wakati mgumu sana katika karne hii ya ukweli na uwazi, kwani kwa sasa huwezi kumdanganya mtu kwani uwezo wa kupata taarifa za kweli umepanuka sana.


Baada ya kuangalia uthibitisho wa maandiko wa ndugu za Ishmael ambao atakaa katikati yake, sasa tutazame ramani jinsi

inavyoonyesha wapi Ishmael aliishi na hao ndugu zake wanavyoonekana katika ramani. Tazama kwa makini.




Ukiitazama ramani ya hapo juu, kwenye ramani chini mwanzo utaona maneno ARABU TRIBES hii ni Shur mahali alipofikia Ishmael na mama yake Hajiri, baada ya kuzaana, watoto wake walitawanyika maeneo mapana ya ukanda wa jangwa la Shur ambalo lilienda hadi Jordan (Edomu –Moabu) hadi Amoni Hadi

Kuweit. Tazama ramani, mishale inaonyesha maeneo walipoishi wana wa Ishmael, utaona Midiani ipo Kusini mwa wana wa Ishmael. Lakini upande wa Mashariki utaona maneno KETURAS SONS NABATU TRIBES hii ni Kuweit ni watoto wa Ketura. Lakini upande wa Kaskazini mwa Ishmael ni Taifa la Israel. Kuangalia vielelezo vya jinsi ya kuisoma ramani tazama ramani ifuatayo.




Kwa mujibu wa ramani ya hapo juu, Makka ipo Kusini, ukiipita Midiani utatembea kilometa 491 kwa gari masaa 5. Na kutoka Midiani hadi Israel kilomita 1238.

**Ukweli upo wazi.**

Kwa mujibu wa maandiko, na kwa mujibu wa vielelezo vya Kijografia ambapo vipo hadi leo, Ishmael wala mama yake Hawajaenda Makka na hili likithibitishwa na Quran kwamba **hajawahi kwenda nabii huko Makka Quran 34:44**, wala malaika hajatabiri kuwa Ishmael ataishi Makka, bali Ishmael aliishi katikati ya ndugu zake, na alifia katikati ya ndugu zake na alizikwa katikati ya ndugu zake.

Mwanzo 25:17.18 *Na hii ndiyo miaka ya maisha ya Ishmaeli, miaka mia na thelathini na saba. Akakata roho, **akafa, akakusanyika kwa watu wake.** Wakakaa toka **Havila mpaka Shur,** unaoelekea Misri, kwa njia ya kwenda Ashuru. Akakaa katikati ya ndugu zake wote.*

Rejea maneno haya “*, **akafa, akakusanyika kwa watu wake.” Kisha rejea maneno haya** “Wakakaa toka **Havila mpaka Shuri,** unaoelekea Misri, kwa njia ya kwenda Ashuru. Akakaa katikati ya ndugu zake wote.”*

Kwamba kuishi hadi kufa Ishmael alikuwa katikati ya ndugu zake. Na cha ziada, Esau alioa mmojawapo wa wana wa Ishmael Tazama Mwanzo 28:9. *Basi Esau akaenda kwa Ishmaeli akamtwaa Mahalathi, **binti Ishmaeli mwana wa Ibrahimu**, ndugu wa Nebayothi, **kuwa mkewe** pamoja na wakeze aliokuwa nao.*

Kwa ufupi, nchi aliyokuwa anakaa Ishmael kwa upande fulani tunaweza kusema ni nchi ya ukweni kwake Edom ambayo baadae ikaunganika ikawa nchi moja ya Jordan.

Tazama ramani ifuatayo, inaonyesha wazi maeneo ya wana wa Ibrahimu ndugu za Ishmael walipoishi. Ukurasa unaofuata





Katika ramani hii wana wa Ishmael hawaonekani kama taifa, kwa ujumla wana Ishamel hawakuweza kujitokeza kwa utambulisho unaojitegemea kama taifa bali walikuwa taifa chini ya taifa. Ndio maana utaona kwenye ramani nyingi hawatambuliki kama taifa linalojitegemea. Katika ramani tunaona eneo lililozunguushiwa alama, hilo ndilo eneo la vizazi vya Ibrahimu ambao waliishi zaidi na kuweka makazi, aidha watoto wa Ishmael waliishi maeneo hayo.

Baada ya hayo tutangalia ramani ya Saudi Arabia tazama hapo mbele




Tunapoingalia ramani ya hapo juu, tunaiona Saudi Arabia. Ijapokuwa majina yanaweza kuwa vigumu kuyatambua kwa ramani iliyotangulia hapo juu ya Saudi Arabia ya sasa, lakini huo ndio muonenako wake na jinsi ilivyopakana na majirani zake hapo zamani. Tazama ramani inayofuata.


© Nations Online Project
N
Mediterranean Sea
Tel Aviv
WEST BANK
Jerusalem
Gaza
Hebron
Baltim
Damietta
Port Said
Arish
Be'er Sheva
Suez Canal
Mansoura
Bir al-Abed
ISRAEL
Negev
Tanta
Ismaïlia
Al Qosimah
Mitzpe Ramon
Banha
Hasna
Nile
Sinai
Wadi Musa (Petra)
Cairo
New Cairo
Suez
Nekhel
Adabiya
JORDAN
EGYPT
Ain Sokhna
Ras Sedr
Eilat
Taba
Aqaba
Fayum
Haql
Beni Suef
Zaafarana
Abu Zenima
Nuweibaa
Biba
Ras Abu Rudeis
Gulf of Suez
EGYPT
Saint Catherine
Mount Sinai 2,285 m
Mount Catherine 2637 m
Dahab
Gulf of Aqaba
SAUDI ARABIA
Ras Ghareb
El-Tor
SINAI (Egypt)
National capital
Governorate capital
Major city
International borders
Sharm el-Sheikh
0 50 100 150 km
0 25 50 75 mi
Hurghada
Red Sea

Ramani hii inaonyesha eneo pana la majirani wa Sauri Arabia.

Ramani ya hapa chini, inaonyesha majirani wa Saudi Arabia na Israel, na maeneo waliyotapakaa wana wa Ishmael. Hii ni ramani ya ulimwengu wa sasa.



Ramani ya Saudi Arabia.





## 3. Wapi Ishmael alioa, au nchi gani ambapo Ishmael aliweza kuoa mke wake?

Kwa mujibu wa maandiko katika kitabu cha Mwanzo 21:20.*21 Mungu akawa pamoja na huyo kijana, naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde. Akakaa katika* ***jangwa la Parani****; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri.*

Jangwa la Parani Lipo Kusini mwa Israel Jangwa hilo la Parani wakati fulani linajulikana kama jangwa la Shur ambalo linaanzia kwenye nyika ya Sinai njia ya kuelekea Misri, ikiwa na maana alikaa katikati ya Israel, Edomo, Misri. Ndio maana mama yake ilikuwa rahisi sana kumtwalia Ishmael mke katika nchi ya Misri. Jangwa la

Shur limeanzia mpakani mwa Misri hadi Jordan hadi Asyria na Kuweit. Kwa hiyo ushahidi huu unaonyesha kwamba, kama angekuwa Makka, haingemuwia rahisi kwa Ishmael kuoa mwanamke wa Kimisri.




Ramani ya nchi ya Misri.





Ukitazama kwa makini ramani ya kwanza iliyoonyesha jangwa la Shur, na ukitazama ramani hii ya pili ya nchi ya Misri, utagundua kwamba, Ishmael na mama yake waliishi mpakani mwa Israel na Misri na upande mwingine alipakana na Edom ambayo kwenye ramani inatajwa kama Jordani kwa sasa. Kwa ujumla tunakubali kuwa, zamani za kale watu pia walisafiri umbali mrefu sana kwa njia zao za usafiri kwa wakati huo, lakini yapo mazingira yanayotukatalia ukweli unaolazimishwa kwamba Ishmael alikimbilia Makka na aliishi Makka yeye na mama yake.

4. **Watoto wa Ishmael waliishi wapi na wapi.**

Ukirejea ramani mbili za mwisho, hiyo ya kwanza yake inaonyesha jagwa la Shuri na mishale kuelekea Haliva ina maana ndio maeneo waliyoishi watoto wa Ishmael walianzia Shur hadi Havila ambayo kwa sasa ni Kuweit. Rejea maandio haya.

Mwanzo 25:17.18 *Na hii ndiyo miaka ya maisha ya Ishmaeli, miaka mia na thelathini na saba. Akakata roho,* ***akafa, akakusanyika kwa watu wake.*** *Wakakaa toka* **Havila mpaka Shur**, *unaoelekea Misri, kwa njia ya kwenda Ashuru. Akakaa katikati ya ndugu zake wote*

*Tazama ramani chini.* ***Havila mpaka Shur***




Kwa kufupisha kabisa, jografia yetu inakataa kukubaliana na dai kuwa Ishmael alikimbilia Makka.

## V. MAelezo kuhusu Makka (kupitia maelezo ya Quran) na nasaba ya Ishmael na Ibrahimu.

Inaelezwa kuwa Hajiri alikimbilia Makka (Kwa mujibu wa Quran Al Baqarah 2:125.127 na ufafanuzi wake) Kisa cha nyumba ya Al Kaaba (Masijid Al Haram) kujengwa na Ibrahimu na Ismail, na kuna vilima viwili ambavyo vipo jirani na msikiti Mkuu uitwao Masijid Al Haram wa Makka (Rejea Quran Al Baqarah 2:158 na ufafanuzi wake na hadithi zake). **Umbali kati ya Safa na Marwa ni takriban mita**

**450 (1,480 ft), kwa hivyo, safari saba za kwenda na kurudi 9za mahujaji kukimbia) ni takribani kilomita 3.6.**


**(Katika kitabu cha Maisha ya Mtume Muhammad cha Shekhe Abdalah Salehe Farisy ukurasa wa 27 kichwa cha habari "kwenda Mirraji" inasema, wakashika njia ya Kaskazini kwenda Baiti,** mwisho wa kunukuu**. Baiti ni Israel ilikuwa Kaskazini mwa Makka, na** Makka ni kusini ya mbali kabisa ya Israel au Kanaani, tunapoongelea Saudi Arabia kwa ujumla inaweza kuingia akilini kidogo kuwa imekaribiana na Palestina, kwa maana imepakana na Jordan  na Jordan imepakana na Israel au Palestina. Lakini Makka ni mbali zaidi kutoka Palestina

**(Katika kitabu cha Maisha ya Mtume Muhammad cha Shekhe Abdalah Salehe Farisy ukurasa wa 29 kichwa cha habari "kwenda Miraji" Nanakuu. " Baiti Muqdas tunakwendwa kwa miezi miwili (siku 60) unajidai (wanamwambia Mtume Muhammad) umekwenda huko kwa usiku mmoja? Mwisho wa kunukuu. )** Aidha katika kitabu **( Cha Histori ya Mtume cha mwandishi Shekhe Othman Maalimu cha 2020 kinathibitisha kuwa Makureishi walimwambia Muhammad kuwa wao wanasafiri kwenda Baiti Muqdas Israil kwa miezi miwili)**

Kwa hiyo, umbali wa kutoka Makka hadi Baiti Muqdas Israel walisafiri kwa siku 60. Ikiwa na maana kwa mujibu wa historia mwendo huu ni wa kutumia wanyama wasio na mwendo wa kasi kama ngamia nk. Kwa hiyo haingii akilini kukubali kuwa Hajiri aliweza kukimbilia Makka kwa umbali huo. Makadirio ya chombo cha maji alichobeba Mwanzo 21:14, inasema Ibrahimu alimpatia kiriba (chupa) ya maji begani mwake na hicho kiriba hakizidi lita 5. Kwa maana Biblia ya Kingereza KJV Inasema alibebeshwa chupa ya

maji (bottle). Kiasi hiki cha maji hata ingekuwa ni lita 5 hakiwezi kutumika kwa siku 60 njiani, ni machache sana. Mara nyingi makadirio ya kiasi cha maji, yanafanana na umbali wa safari.

Saudi Arabia ipo kusini mwa Israel, lakini ukiwa Makka Israel inakuwa Kaskazini mwa Makka hivyo historia au Jografia ya Kiislamu na Biblia ni sawa. Tazama ramani na pembe za ramani kujua Makka ni upande gani wa Israel





Kwa mujibu wa ramani kusini ni Saudi Arabia ambapo Makka ipo mwisho wa nchi ya Saudi Arabia.

Tazama ramani ya Saudi Arabia chini. Makka ipo karibu na mwisho wa Saudi Arabia




Imepakana na bahari ya Red sea. Muonekana wa Msikiti wa Makka na ramani ya vilima Safa na Marwa na Kisima cha Zamzama.

tazama vielelzo vya mbele.




Hii ni ramani ya eneo la Hijja la huko Makka. Ni kwa ujumla wake matukufu yote muhimu ya Waislamu yapo jirani jirani na Makka. Labda tungeambiwa Safa na Marwa ipo Madina nahata hivyo sio

jirani na Israel, lakini Makka ni mbali mno na kiukweli mji wa Makka na Msikiti wa Al Haram na Kaaba kwa ujumla haina uhusiano wowote na Ishmeil wala Ibrahimu wala Hajiri, kwa ujumla Hajiri hajawahi kwenda huko kabisa wala Ibrahimu wala Ishmael. Kwa hiyo tunahitimisha mada hii kwa kusema kwamba, Makka na Kaaba na msikiti wa Makka hauna uhusiano na familia ya Ibrahimu.

**Yafuatayo ni majibu ya Wayahudi kuhusu Makka** je wanalijua hilo kama Makka imejengwa na Ibrahimu na Ishmael?

Maswali waliyoulizwa Wayahudi kuhusu msikiti wa Makka kujengwa na Ibrahimu na Ishmael, kupitia chombo cha habari Israel, walijibu hilo halipo, kwa kuwa baba yao Ibrahimu aliishi kwenye mahema hadi kufa kwake hajawahi kujenga nyumba hata yake mwenyewe. Leo watasemaje kuwa Ibrahimu kajenga nyumba? Fuata link ya hapa chini kusikiliza youtube. Tafuta. **Religious Israelis: Who built the Kaaba?**
https://www.youtube.com/watch?v=vO2WPMho5pQ&t=6s